

## MPIGA ZEZE

### E. Kezilahabi

Nitaimba wimbo gani tofauti na za zamani?  
Je nitaeleza kisa cha kichaa  
Aliyepotea njia akagonga mlango  
Wa nyumba yake kuuliza?  
Au cha Anastazia msomi  
Aliyeiba senene waliokaangwa?  
Mtaniita mwongo nikiwambia  
Kuwa Deusi alikufa kimzaha  
Roho yake ilitoka Pap! Ikaepuka  
Harufu mbaya ya zizi la ng'ombe  
Na kutokomea gizani ikitabasamu  
Na kusindikizwa na kwaya ya kunguru  
Waliomcheka Padiri aliyeleta Sakramenti  
Ungekuwapo kumwona ndama aliyezaliwa  
Akalambwa na mamaye kisha akasimama  
Akayumbayumba kutafuta ziwa shingoni  
Ni mimi mpiga zeze kipofu wa kijijini  
Nikilewa naimba matusi  
Nimewahi kuvunja buyu mara tatu  
Mto Nabili ulifurika kwa mvua ya juzi  
Ukamchukua mama mja mzito  
Aliyebeba mzigo kichwani, mtoto mgongoni  
Nilikuwapo Maira alipoliwa na simba  
Alipiga kelele kama mbuzi  
Hadi simba alipong'oa ulimi wote  
Kuzima domo lake pana  
Na wewe Nyangere unaringa nini  
Una shanga mbili kiunoni za kuazima  
Hata Nyamchele anakuzidi  
Wenzio wako mazikoni, wewe ndani  
Ya nyumba duduliduduli na mumeo  
Nilikwenda mjini kumtembelea Mazula  
Wakaleta ugali na samaki nikala pyuu  
Watoto wakamlilia mama yao  
Leo tutalala njaa, kuna fisi mezani  
Kumbe chakula cha watu kumi!  
Na wewe Nyachiro hujui Sikamoo Malaaba  
Ukienda mjini na shanga nyingi  
Utapigwa na kina Amina!